MUHTASARI WA MAAZIMIO NA MAPENDEKEZO YATOKANAYO NA KONGAMANO LA 7 LA KISAYANSI LA WATAALAMU WA MAGONJWA YA FIGO TANZANIA (NESOT)

TAREHE 25-26, NOVEMBA, 2021

RAMADA HOTEL, DAR ES SALAAM

MGENI RASMI: Mh Dr Jakaya Mrisho Kikwete – Rais Msaafu wa JMT

MGENI MAHSUSI: Dr Tegetsu Ketsela Mengestu- Mwakilishi Mkazi-WHO

WAALIKWA MAALUM:

1. Dr Omary Ubuguyu- Kaimu Mkurugenzi-Tiba (WAMJJWW)
2. Dr James Kiologwe- Naibu Mkurugenzi- Magonjwa Yasiyoambukiza (WAMJJWW)
3. Dr Rashid Mfaume –Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam
4. Sheikh Alhadi Mussa Salum- Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam
5. Mch Charles Mzinga – Mchungaji, KKKT, Mashariki na Pwani
6. Washiriki Mahsusi: Dr Twahir na Dr Sokwala (Kenya), Dr Tannor (Ghana), Dr JanMohamed (Uingereza)
7. Viongozi waandamizi wa NESOT
8. Wataalamu wa Figo; Kanda zote za Tanzania, Mashariki, Zanzibar, Kaskazini, Kati, Ziwa, Kusini, Nyanda za Juu na Magharibi.
9. Wadhamini, Wafanya Maonesho na Waandishi wa Wahabari
10. Wanafunzi, Wasaidizi, Mabibi na Mabwana

Yatokanayo:

A. Ushauri na Mapendekezo toka kwa Mgeni Rasmi:

1. Tujipongeze kwa kupiga hatua kubwa sana katika kuendeleza afua za afya ya figo hapa nchini ndani miongo michache iliyopita
2. Nafarijika kuona mafunzo ya kibingwa na kibobezi ya magonjwa ya figo kwa kiasi kikubwa yanapatikana hapa Tanzania kwa sasa
3. Sambamba na mafanikio hayo, tuendeleze mashirikiano ya kitaalamu, kitiba na kitafiti na wadau wetu wa maendeleo waliotushika mkono mpaka kufika tulipofika na tukaribishe wengine ili kuimarika zaidi
4. Afua ya kinga (hususani katika ngazi ya jamii), ipewe kipaumbele ili kupunguza idadi na kasi ya wagonjwa wanaohitaji matibabu ya mwisho na ya lazima (kusafisha damu, kupandikizwa) kwani hatua hizi zina gharimu sana wagonjwa,familia na serikali kwa ujumla.
5. Kwa sasa ambapo uwekezekaji kwenye vifaa tiba umefikia kiwango cha kuridhisha, kipaumbele kiwe kwenye upatikanaji (kufikika, kupata na kumudu gharama) ya huduma za figo nchini
6. Ili kufanikisha upatikanaji wa huduma hizi muhimu kwa wagonjwa; tuiunge mkono na tuishauri serikali namna bora ya kuingia katika mfumo wa bima ya afya kwa wote (Universal Health Care).
7. Tunashukuru Upandikizaji wa figo kwa sasa unafanyika hapa nchini: tuendelee kujifunza namna ya kuimarisha matibabu haya ili kupunguza uwezekano wa figo kukataliwa (rejection) hususani zinazotokea mapema baada ya upandikizaji.
8. Tuendelee kutoa ushauri wa kitaalamu na ushauri kwa serikali ili iendelee kuwekeza kwenye maeneo ya kipaumbele katika afua anuai za afya ya figo .
9. Kuhakikisha kuwa maazimio yanayotokana na makongamano yetu ya figo, yanaifikia serikali kupitia wizara katika namna ambayo inarahisisha na kuharakisha utekelezaji wake kwa namna inayopimika

10. Kurejea utekekelezaji wa maazimio yaliyopita na kupima tija (impact) ya mapendekezo mliyoyatoa katika kongamano lililotangulia (mf; kutengeneza miongozo ya matibabu ya figo au kuboresha sera za afya ya huduma za afya ya figo nchini).

B. Mapendekezo yaliyotokana na Uwasilishaji wa Mada Mbalimbali

<u>Uwasilishaji kwa njia ya Mabandiko (Posters):</u>

1. Kuna uhusiano mkubwa kati ya ugonjwa wa malaria na mshtuko wa ghafla wa figo (Acute Kidney Injury). Wataalamu wanashauriwa kuwa makini na uhusiano huu na kutoa matibabu thabiti kwa ugonjwa wa malaria mapema kabla haujaelemea figo.
2. Ubora wa maisha kwa wagonjwa wa figo wanaosafishwa damu upo chini na jambo la kuzingatia tunapotoa huduma kwa wagonjwa hao.
3. Tiba-lishe ni muhimu katika kukamilisha matibabu mtambuka wa magonjwa ya figo. Tuhakikishe tunashirikisha wataalamu wa tiba lishe katika maamuzi yetu ya kila siku tunapotoa huduma kwa wagonjwa wetu wa figo.
4. Ugonjwa wa mshtuko wa ghafla wa figo (Acute Kidney Injury) huathiri hususani vijana (ambao ndio nguvu kazi ya Taifa) hususani wanawake. Malaria,homa ya mapafu, maambukizi ya bakteria na madhara yatokanayo na ujauzito ni magonjwa yanayohusishwa na mshtuko wa ghafla wa figo kwa hivyo tahadhari zaidi zichukuliwe tunapohudumia wagonjwa hao.
5. Maumivu ya kichwa hutokea mara kwa mara kwa wagonjwa sugu wa figo wanaosafishwa damu. Maumivu haya ya kichwa yana vyanzo tofauti kwa wagonjwa tofauti. Ni muhimu kutafuta chanzo mahsusi kwa kila mgonjwa na kukitibu

6. Wauguzi ni nguzo muhimu katika matibabu ya figo. Watafute kwa kupewa nafasi za masomo ya juu na kujiendeleza wakiwa kazini na washiriki kwenye makongamano kama haya ili wapate fursa ya kuongeza ufahamu wa maendeleo mapya katika sekta zao.

Uwashilishaji kwa njia ya Maongezi (Oral Presentation)

Matibabu ya Figo katika Enzi za Janga la UVIKO-19:

UVIKO-19 umeathiri kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma za figo na bado hakuna muafaka katika miongozo thabiti ya kutuongoza katika namna ya kuhudumia wagonjwa wa figo (katika kliniki,wanaosafishwa damu na waliopandikizwa figo).
Hivyo basi, kwa sasa tunategemea zaidi kujifunza kwa kubadilishana uzoefu.
Katika Kongamano hili tumealika wataalamu toka nje ya nchi ili kubadilishana uzoefu

1. **Uzoefu toka Kenya**

   - Matibabu ya Masafa (Telemedicine) yamesaidia sana kuhudumia wagonjwa katika kipindi cha UVIKO-19

2. **Uzoefu toka Uingereza**
   - Kupata chanjo dhidi ya UVIKO-19 mapema kunapunguza sana nafasi ya kulazwa hospitali na kupata madhara makubwa (complications) za UVIKO-19
   - Kwa wagonjwa waliopandikizwa figo baadhi ya dawa (antimetabolites) zisimamishwe na dawa nyingine (CNIs) zipunguzwe

dozi ili kulinda figo iliyopandikizwa na maisha ya mgonjwa kwa ujumla wake

3. **Uzoefu toka Ghana**
   - Miongozo Thabiti ya matibabu ya wagonjwa wa figo enzi hizi za UVIKO-19 haijakamilika.

4. **Uzoefu toka Tanzania**
   - Tuendelee kuhamasisha chanjo na kushiriki katika tafiti za kikanda na za kimataifa ili kupata miongozo ya matibabu kwa wagonjwa hao.
   - Wauguzi wapo mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Mafunzo ya kuhudumia na vifaa vya kujikinga (PPE) dhidi ya UVIKO-19 ni muhimu mno.

SIKU YA PILI YA KONGAMANO

1. Afua ya ung”amuzi wa magonjwa ya figo kwa kuchukuwa sampuli (Nephropathology) imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza uhakika wa ugonjwa (diagnosis) pamoja na kuongoza matibabu (guide therapy) na kubashiri matokeo (prognosticate) matibabu ya magonjwa anuai ya figo

2. Uwekezaji zaidi unatakiwa ili kuweza kupata vifaa vya ubora zaidi katika ung”amuzi na mafunzo zaidi (ya muda wa kati na muda mfupi) katika wataalamu wa patholojia ya figo unahitajika sana ili kuongeza wigo na tija ya tasnia hii muhimu.

3. Matumizi ya kisukari kwa kutumia dawa mpya za kutibu aina ya SGLT-2 inhibitors imethibitishwa kuwa na manufaa dhidi ya

ugonjwa wa figo utokanao na kisukari. Ni vema Mamlaka husika zikijikita katika kununua na kusambaza dawa hizi na kurahisisha upatikanaji wake kwa wagonjwa hao.

4. Ni vyema kuhakiki usugu wa ugonjwa shinikizo la juu la damu (Resistant Hypertension) na shinikizo –bandia sugu la juu la damu (pseudoresistant) kabla ya kupanga mkakati wa matibabu

5. Upungufu wa damu kwa wagonjwa sugu wa figo ni tatizo kubwa na utafiti zaidi unahitajika katika kungamua vichochezi na visababishi miongoni mwa wagonjwa wetu

6. Uwekezaji zaidi unahitajika katika mafunzo kwa madaktari wa upasuaji wa mishipa (arterio-venous fistula) na kwa wauguzi kuhusu matunzo na matumizi sahihi ya fistula hizo ili kuongeza tija na ubora wa huduma ya usafishaji wa damu (dialysis)

7. Uwekezaji katika teknolojia na mafunzo katika tiba bora ya usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo (adequate dialysis) ni muhimu katika kuimarisha ubora wa matibabu, kupunguza madhara na kupunguza vifo miongoni mwa wagonjwa wa figo

8. Uwekezaji zaidi na mafunzo zaidi ya tiba mbadala ya ugonjwa sugu wa figo (usafishaji damu na upandikizaji figo) kwa watoto unahitajika sana na huu ni wakati muafaka wa kufanya uwekezaji huu ili kupunguza vifo vya watoto.

9. Miongoni mwa wagonjwa sugu wa figo waliopo kwenye matibabu ya usafishaji wa damu , ugonjwa wa tezi ya parathyroid upo zaidi kwa wale wenye shinikizo la juu la damu na wanaofanyiwa usafishaji wa figo mara chache zaidi ya inavyoshauriwa

10. Uwekezaji zaidi unahitajika katika teknolojia ya usafishaji wa damu kwa njia ya utando wa tumboni (peritoneal diagnosis) kwani ni rahisi na inaongeza wigo wa mazingira ya kupata huduma hii

11. Ili kuimarisha programu ya upandikizaji wa figo hapa nchini; kurasimishwa kwa sheria,taratibu na miongozo ya huduma hii, kuboreshwa kwa maslahi ya watumishi na uwekezaji zaidi kwenye teknolojia na mafunzo ya wataalamu anuai wanaohitajika ili kufanikisha huduma hii.

12. Mliganjo wa lishe kwa wagonjwa wa figo ni suala muhimu sana ili kuepuka ziada huku ukiepuka madhara ya lishe duni hususani kwa wagonjwa wanaosafishwa damu !

13. Matibabu ya Figo yanayolenga kumjengea uwezo mgonjwa (Patient Centred Care) yanasaidia sana katika kumrejeshea mgonjwa ubora wa maisha, kupunguza utegemezi na kuongeza na ushiriki wake katika jamii yake.

14. Ubora wa huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa sugu wa figo unaweza kuongezwa kwa kuimarisha mipango binafsi ya matibabu ya figo (individualized treatment plan) kwa kila mgonjwa

15. Mawasiliano Mahsusi kwa njia ya Kikundi Sogozi Whatsapp (Whatsapp Group) yanaweza kutumika miongoni mwa katika kuboresha mawasiliano baina ya wauguzi wanaotoa huduma ya wagonjwa sugu wa figo wanaosafishwa damu.

16. Utapiamlo, upungufu wa damu na kupungua kwa tija ya moyo (Heart Failure), matatizo ya mifupa, hutokea kwa wingi miongoni mwa wagonjwa sugu wanaosafishwa damu. Madhira haya hupunguza ubora wa maisha na huongeza gharama za matibabu kwa wagonjwa hawa na serikali kwa ujumla. Uwekezaji zaidi na mafunzo vinahitajika ili kungamua mapema na kuyatibu mapema madhira haya.

17. Kwa kushirikiana na WAMJJWW, Chama cha Wataalamu wa Figo Tanzania (NESOT) ipo tayari kusaidia kujenga uwezo wa hospitali za kanda na mikoa katika kuhudumia wagonjwa wa figo (wanaosafishwa damu, walioapandikizwa figo nk) mpaka kufikia hatua za kuanzisha program hizo katika hospitali hizo. Tunaomba tuhusishwe, tushirikishwe na tuwezeshwe ili tuandae rasimu ya mpango-kazi huo ambao utaainisha namna ya utekelezaji wa mpango mkakati huo !

Tunawasilisha kwa kumbukumbu na utekelezaji !

Dr Onesmo Kisanga

Rais- NESOT

26.11.2021